
# Uendelezaji wa Vikundi vya Wakulima

## Kanda ya Mashariki







MKL
HD1486
.T34
U6

TARP II SUA PROJECT

UENDELEZAJI WA

# VIKUNDI VYA WAKULIMA

KANDA YA MASHARIKI

**Warsha ya Nane ya Wakulima wa Kanda ya Mashariki**
**Iliyofanyika Ukumbi wa CCM, Lushoto, Tanga**

**21-23 Juni 2004**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima
Wadogowadogo Tanzania

***(TARP II-SUA Project)***

**Kimeandikwa na**

Bi. Fausta Vallery
Bw. Philemon Kawamala
Prof. Rogers. E. Malimbwi
Dk. Joyce G. Lyimo-Macha

**Kimehaririwa na**

Prof. L. D. B. Kinabo - Mratibu wa Mradi

**ISBN: 9987-422-06-3**

**Kimechapishwa na**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima
Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 /1102

Chapisho namba: TS2-116

©Haki ya kunakili -- TARP II SUA Project, 2005

# Yaliyomo


**Dibaji** v
**Vifupisho** vii

**1.0 UTANGULIZI** 1
1.1 Ufafanuzi wa maneno muhimu 2
1.2 Matarajio ya wanawarsha 3
1.3 Mbinu zilizotumika 4

**2.0 UUNDAJI WA VIKUNDI NA SABABU ZAKE** 8
2.1 Uundaji vikundi 9
2.2 Mambo ya kuangalia katika uundaji 10
2.3 Ukuaji wa kikundi 11
2.4 Uundaji wa mtandao 13

**3.0 MISINGI YA VIKUNDI BORA** 13

**4.0 UONGOZI BORA WA KIKUNDI** 14
4.1 Mambo ya kuzingatiwa na uongozi wa kikundi 15
4.2 Sifa za kiongozi 15

**5.0 UENDESHAJI WA KIKUNDI** 15
5.1 Katiba ni nini? 15
5.2 Ushirikishwaji wa wanakikundi 16
5.3 Umuhimu wa vikao kwa wanachama 17
5.4 Idadi ya wanachama katika kikundi 17
5.5 Uwezo wa kikundi 17
5.6 Mawasiliano kati ya viongozi na wanakikundi 18

**6.0 TABIA NA MIGONGANO KATIKA VIKUNDI** **18**
6.1 Maana ya tabia 18
6.2 Migongano katika kikundi 19

**7.0 WAJIBU WA WANAKIKUNDI NA KAMATI YAO** **21**
7.1 Muundo wa kamati 21
7.2 Wajibu wa kikundi 21
7.3 Wajibu wa kamati ya kikundi 22

**8.0 HITIMISHO** **22**
8.1 Mpango wa kazi 22
8.2 Mapendekezo ya kuboresha vikundi 23
8.3 Tathmini ya warsha 23
8.4 Kufunga warsha 24

**9.0 VIAMBATISHO** **25**
9.1 Orodha ya washiriki 25
9.2 Jinsi watu wanavyokutana 28
9.3 Mipango ya utekelezaji wa kazi 29

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS), na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza mradi wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi mwezi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway.

Kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kutekeleza malengo ya mradi na kuimarisha uhusiano na wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

- Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo na ufugaji
- Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo
- Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele
- Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo na mifugo.

Chapisho hili linawasilisha mwenendo wa Warsha ya nane ya wakulima wa Mikoa ya kanda ya Mashariki kuhusu **Uendelezaji wa Vikundi vya Wakulima** iliyofanyika ukumbi wa CCM, Lushoto, Tanga, 21-23, Juni 2004. Mwenendo wa warsha umechapishwa na kutolewa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

*Prof. L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| AHI | Mradi wa Kilimo cha Milimani |
| ARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo |
| HUSETA | Shirika la Makazi ya Jamii Tanzania |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Chakula |
| NGO | Shirika lisilo la Kiserikali |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| SECAP | Mradi wa Kuhifadhi Ardhi na Kilimo Mseto |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |

# 1.0 UTANGULIZI

Warsha iliandaliwa na Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP 11-SUA Project) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS) pamoja na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Lengo kuu ni kuimarisha uhusiano kati ya wakulima, watafiti na wataalamu wa ugani na pia kuwawezesha washiriki watambue hali ya vikundi vyao na pia waweze kuwa na mikakati ya uboreshaji ili kufanya vikundi kuwa endelevu.

Washiriki wa warsha walitoka mikoa ya Dar-es-salaam, Morogoro, Tanga, Pwani na Mbeya ambayo iliwakilishwa na vikundi 7 vya wakulima. Kati ya hivyo vipo vikundi vinavyoshirikiana kufanya utafiti na SUA chini ya mradi wa TARP 11-SUA. Washiriki wengine walitoka katika taasisi zisizo za kiserikali (NGO), wataalamu wa ugani, watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ARI)- Uyole na SUA na kufanya jumla ya washiriki kuwa 30. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo; Wakulima 15 (Ke 9), wataalamu wa ugani 3, watafiti 5 (Ke 2) kutoka ARI- Uyole, ARI-Mikocheni, ARI-Cholima, na ARI-Mlingano. Wawakilishi kutoka NGO walitoka SECAP na AHI, Lushoto na mwingine HUSETA. Orodha ya washiriki na anuani zao ipo katika Kiambatisho Na.1.

Madhumuni ya warsha yalikuwa ni:

- Kuwezesha washiriki kujua na kutumia mbinu mbalimbali katika kuanzisha na kuendeleza vikundi vyao na vile vile kuwawezesha wanavikundi wao wenyewe kuweza, kuainisha na kutathmini malengo na shughuli za vikundi kwa ujumla.
- Kuwawezesha washiriki kuandaa mpango wa utekelezaji wa miradi mbali mbali kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira yao

Kuwepo kwa vikundi vyenye shughuli endelevu ni moja ya mkakati wa utekelezaji wa mkakati wa taifa ambayo mtu binafsi, makundi mbalimbali, mashirika ya serikali na yasiyo ya serikali kuweza kupambana na umaskini uliokithiri katika jamii ya watanzania. Kuhakikisha kuwa wanajamii wanaondoa tatizo la üpungufu wa chakula katika kaya zao na kujiongezea kipato kutokana na rasilimali zinazowazunguka ni moja ya mikakati inayotekelezwa na TARP II-SUA ili kuboresha ustawi wa jamii katika kanda za Mashariki na Nyanda za Juu Kusini.

Ni wazi kwamba tunaweza kujikwamua katika umasikini kwa haraka iwapo tutawawezesha wananchi kuunda vikundi endelevu katika kuzalisha mazao mbali mbali na kuimarisha masoko ya mazao hayo. Hivyo basi hatuwezi kuwa na vikundi imara kama vikundi hivyo havitakuwa na mbinu mbali mbali za uzalishaji, kujipatia masoko na vile vile kuainisha maeneo ya kupata mafunzo ili viweze kujiendesha kwa ufanisi.

**Angalizo:** *Shughuli mbalimballi zinazowezeshwa na TARP 11 SUA ni hatua ya makusudi ya utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini hapa nchini.*

## 1.1 Ufafanuzi wa maneno muhimu

Ili kuwezesha washiriki kuelewa zaidi, ufafanuzi wa maneno yafuatayo ulifanyika

**Kikundi:** Ni ushirikiano wa watu walioamua kwa hiari yao wenyewe kujiunga pamoja kwa nia ya kutatua matatizo yao

**Mtandao wa vikundi:** Ni muungano wa vikundi mbalimbali katika ngazi mbalimbali, kwa mfano: kijiji, kata, tarafa, wilaya, mikoa na taifa

**Katiba:** Ni taratibu, desturi au kawaida, zilizo za lazima ambazo zinatumika kama mwongozo katika uendeshaji wa shughuli.

**Uongozi:** Ni utaratibu unaowekwa ili kusaidia, kusimamia na kuratibu shughuli za kikundi

**Migogoro/migongano katika vikundi:** Migogoro hujitokeza pale pande mbili au zaidi zinapoona kwamba nia ya kupata madaraka au mali, kushiriki katika kutoa maamuzi dhidi ya maslahi ya jamii hayawezi kufikiwa kwa wakati au zinapotambua tofauti katika mahitaji, utashi, na imani

**Mtaalamu wa ugani:** Ni mtumishi aliyeajiriwa ili kutoa ushauri wa kitaalamu wa aina mbalimbali kwa jamii ili utumiwe katika maisha ya kila siku. Watumishi kama Afisa maendeleo ya jamii, Kilimo, Afya, Mifugo huitwa maafisa ugani

**NGO:** Ni taasisi isiyo ya kiserikali, inayofanya kazi kufuatia utaratibu iliyojiwekea ambao unawiana na sera za nchi, zenye lengo la kuwezesha jamii kuboresha hali ya maisha

**Mtafiti**: Ni mtu anayefanya uchambuzi wa kina katika kubaini matatizo au vikwazo vilivyopo katika jamii vya uendeshaji wa maisha ya mwanadamu na kubuni au kupendekeza utatuzi wake

## 1.2 Matarajio ya wanawarsha

Ili kuelewa na kuainisha mahitaji ya wanawarsha, kila mshiriki alichangia kwa kutoa matarajio yake kama ifuatavyo:

- Kuelewa jinsi ya kuimarisha vikundi vilivyopo kanda ya Mashariki
- Kubadilishana uzoefu na ujuzi kutoka kwa washiriki wa maeneo mbalimbali na shughuli zinazofanyika
- Kupata elimu zaidi na mbinu za kuendesha na kuimarisha vikundi
- Kupata mbinu mpya za kukuza uzalishaji wa kilimo na mifugo
- Kujifunza mbinu za kuendesha vikundi
- Kupata mafunzo ya msingi ya kuimarisha vikundi vya ufugaji mbuzi wa maziwa,
- Kupata mbinu ya kufanya vikundi vya ufugaji wa kuku wa kienyeji kuwa endelevu
- Kupata mafunzo ya kilimo bora

- Kujifunza namna vikundi vinavyofaidika na kilimo kufuatia mradi wa TARP II-SUA
- Kupata mafunzo hapa na kwenda kuwaelimisha wenzangu waliobaki nyumbani
- Kupata mafunzo ya jinsi ya kufanya kazi za vikundi kuwa endelevu
- Kupata mbinu za kutosheleza chakula katika kaya
- Kupata mafunzo ambayo siyaelewi
- Kujifunza mambo mbalimbali ya kujiendeleza

## 1.3 Mbinu zilizotumika

Mbinu shirikishi ilitumika ili kila mshiriki kupata nafasi ya kuchangia kwa uhuru zaidi. Njia zilizotumika ni pamoja na:

- Majadiliano katika vikundi ambapo vikundi viligawanywa na kuwa na vikundi vitatu; wakulima, wataalamu wa ugani, na wanawake.
- Vibwagizo kama vile nyimbo vilitumika
- Michezo kama kuzama boti na kushindania kiti cha kukalia
- Michoro ya chapati katika kutambulishana, na ya wanyama wanaovutana

Njia hizo zote ziliwezesha washiriki kuweza kutambua na kulinganisha mazingira yao juu ya maendeleo ya vikundi na jinsi vinavyoweza kujikwamua na kuwa endelevu.

### *1.3.1 Majadiliano katika vikundi*

Washiriki walibadilishana uzoefu kutoka maeneo mbalimbali yaliyowakilishwa kwenye warsha, ambapo washiriki walitakiwa kutoa uzoefu wao kuhusu maendeleo ya vikundi wakichambua uwezo na udhaifu wa vikundi, na hatua zinazochukuliwa ili kufanya vikundi kuwa endelevu na kisha kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha vikundi vyao.

### *1.3.2 Taarifa za vikundi*

Washiriki walitoa changamoto mbalimbali kwa kurejea maeneo wanayotoka kama ifuatavyo:

## Kikundi cha Umoja – Wakulima wanaume

| Uwezo/Nguvu | Udhaifu |
|---|---|
| • Baadhi ya vikundi kama vile kikundi cha KIWAMIPA vina akaunti benki<br>• Vikundi vya Vuga na Mgeta wameanzisha mchango ili wafungue akaunti<br>• Kutengeneza vitu mbalimbali kwa kutumia unga wa mhogo kama vile kutengeneza vibabu, unga, maandazi, chapati, chipsi kwa ajili ya kuuza na chakula (Songabatini)<br>• Kufuga mbuzi wa maziwa na kutumia maziwa yake kwa familia (Mgeta)<br>• Baadhi ya vikundi vina uongozi uliokamilika<br>• Wanakikundi wanatunisha mfuko kwa kuchangia kila mwezi (Vuga)<br>• Wanavikundi kutembeleana na kusaidiana katika ufugaji<br>• Kukutana kila mwezi | • Katiba haijaundwa<br>• Vikundi havijasajiliwa |

**Hatua za kuchukuliwa**
Wataalamu watembelee vikundi na kutoa ushauri mara kwa mara

**Kikundi cha Juhudi – Wakulima wanawake**

| Uwezo/Nguvu | Udhaifu |
|---|---|
| • Wanao mbuzi na ng'ombe wa maziwa wanaowapatia maziwa kwa matumizi ya familia na kuuza<br>• Baadhi ya vikundi vina akaunti benki (Twabaha na Mwamko)<br>• Baadhi ya wanavikundi wanao uwezo wa kuendeleza teknolojia ya ufugaji wa mbuzi wa maziwa<br>• Baadhi ya vikundi vina katiba<br>• Baadhi ya vikundi vinatunza kumbukumbu kama vile daftari la muhtasari na mahudhurio, fedha, mauzo, mikopo<br>• Kikundi cha Songabatini kina mashine ya kusindika vyakula<br>• Kikundi cha MUWAMU Muheza kinazalisha mazao yenye kiwango kinachokubalika na TBS | • Wanakikundi hawana elimu ya kutosha kuhusu vikundi, kubuni miradi, uongozi, na jinsi ya kutunisha mfuko wa kikundi<br>• Wanakikundi kutohudhuria mikutano<br>• Kukosa vitendea kazi kama vile vifaa vya kumwagilia, kupimia mifugo kama vile ng'ombe na mbuzi<br>• Kukosa jengo la kufanyia shughuli za kikundi |

**Hatua za kuchukuliwa**

Kuendelea kuhamasishana kwenye kikundi na pia kuhamasisha watu wengine wanaopenda kujiunga na vikundi.

**Kikundi cha Motomoto – Wagani/Watafiti**

| Uwezo/Nguvu | Udhaifu |
|---|---|
| • Kuhamasisha na kuunda vikundi vya shughuli mbalimbali<br>• Kushawishi wanavikundi kutumia nguvu zao na rasilimali zinazowazunguka katika kutatua matatizo yao<br>• Kuibua na kueneza ujuzi/utaalamu katika maeneo mbalimmbali | • Wanavikundi kutegemea misaada zaidi<br>• Kukosa nyenzo ili kuwafikia wakulima<br>• Elimu ya uongozi ni ndogo katika vikundi<br>• Baadhi ya viongozi kutokuwa wazi kuhusu masuala ya maendeleo ya kikundi<br>• Huduma za ugani kutowafikia walengwa kwa wakati muafaka<br>• Ushirikishwaji mdogo wa fani mbalimbali kwa sababu ya mfumo uliopo wa utendaji kazi na uwezo mdogo kifedha |

**Hatua za kuchukuliwa**

Kikundi cha motomoto (wagani/watafiti) nacho kilipendekeza mambo yafuatayo;

- Kushirikisha taaluma mbalimbali katika kuanzisha na kuendeleza vikundi
- Kuwepo na mtandao wa vikundi vya ndani na nje
- Mafunzo yatakayokuwa yanaandaliwa yalenge mahitaji muhimu ili kikundi kiwe endelevu
- Kutoa elimu ya uzalishaji, masoko, uendeshaji na uimarishaji wa vikundi
- Kuwezesha vikundi vijisajili na kuwa na akiba benki.

## 2.0 UUNDAJI WA VIKUNDI NA SABABU ZA KUUNDA

Washiriki walitoa sababu kuu za wao kujiunga kwenye vikundi kama ifuatavyo:

- Kutatua matatizo au haja zilizopo
- Kufanya kazi kwa pamoja
- Kuongeza ushirikiano
- Kuharakisha utendaji wa kazi
- Kurahisisha huduma na kutambulika
- Kujifunza kwa wengine
- Kuongeza mapato na kugawana faida

Ni kweli mtu yeyote anayefanya kazi kwa kutegemea mawazo yake peke yake siyo rahisi kupata maendeleo ya haraka. Watu wengi wanaposhirikiana pamoja, huweza kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja. Pia kwa kufanya kazi pamoja watu wanaweza kufikia malengo waliyopanga kwa urahisi. Ili kikundi kiwepo na kiwe imara na endelevu lazima mambo makuu yafuatayo yawepo:

- Watu
- Uhusiano mzuri na imara baina yao
- Kujitolea kwa hiari kufanya kazi
- Uwazi katika kuendesha kikundi

Uzoefu wa wanavikundi umeonesha kuwa vikundi vingi vimeanzishwa ili kupata msaada kama vile mikopo na mara nyingi vikundi kama hivyo husambaratika hali ikiwa kinyume na matarajio. Ili tuwe na vikundi endelevu ni bora tuunde vikundi vinavyolenga kutatua matatizo yanayotukabili katika maisha yetu ya kila siku. Vikundi vyenye nafasi kubwa ya kudumu ni vile vinavyoundwa na wanajamii kwa hiari yao wenyewe na wanajamii wakijua kuwa wao ndio wamiliki wa vikundi hivyo kwa kutatua matatizo yao wenyewe. Imebainishwa kuwa vikundi vilivyoanzishwa bila kuibua changamoto na hatimaye kujiwekea

mipango ya kupambana na changamoto hizo bado vina nafasi ya kufanya marekebisho ili viweze kuwa endelevu.

**Angalizo:** *Inabidi kikundi kuwa na lengo na mpangilio mzuri wa shughuli mbalimbali za kiuchumi au za huduma. Jambo muhimu la kukumbuka ni kwamba inabidi kujiuliza kuwa anayeunda kikundi ni nani na ni mali ya nani, na wazo linatoka wapi, na kitu gani kinachosababisha kuunda kikundi. Pia ni kwa jinsi gani vikundi vinafanya kazi ndani ya uwezo uliopo.*

## 2.1 Uundaji vikundi

Kujiunga kwenye kikundi ni kitu cha hiari, pia hufanywa na watu wenyewe. Na kwa hiyo wazo la kuunda kikundi hutokana na mtu mmoja/watu wachache tu wakati kuna tatizo linalohitajika kutatuliwa. Kikundi kinaweza kuundwa pia na watu wenye mahitaji tofauti na mitizamo tofauti lakini wakaweza kusawazisha tofauti zao na kuwa na mtizamo mmoja.
Kikundi kinachoundwa kinaweza kuwa cha:

- Uchumi
- Huduma

Uzoefu umeonesha kuwa vikundi vingi hufa baada ya kuanza, kwa sababu wanakikundi huamua bila kutambua malengo ya kuwa kwenye kikundi, na hivyo kupelekea wanachama kutotimiziwa matakwa yao na vile vile vikundi vingine huanzishwa na miradi moja kwa moja bila matayarisho na bila kuchambua matatizo, mawazo na mazingira ya wanajamii. Ni muhimu kabla ya kuunda kikundi kuwashirikisha wanajamii kutoa changamoto zao na vile vile kujiwekea mikakati ya kupambana na changamoto hizo.

**Je ni kitu gani kinafanya kufikia kuunda kikundi?**

Ikumbukwe kwamba kuanzisha kikundi ni kitu cha hiari na hufanywa na watu wenyewe na wala siyo kwa shinikizo kutoka nje. Aidha uzoefu umeonesha kuwa vikundi vingi vinavyoanza kwa shinikizo toka nje mara nyingi uwajibikaji unakosekana na utegemezi uliokithiri hujitokeza hali ambayo hupelekea vikundi kuwa na shughuli zisizokuwa endelevu. Ili kufanikiwa watu wenyewe waamue kuunda vikundi vyao na wao wenyewe waweke mikakati ya jinsi ya kuviendeleza.

Ili kikundi kiweze kuundwa na kujiletea mafanikio ni vyema wale wanaounda kikundi wawe na malengo ya aina moja na yanayokubalika na kuzingatiwa na wanakikundi wote. Maana wakiyafahamu watakuwa na ari ya kuyatekeleza ili yafanikiwe. Kutokana na hali hiyo masuala yafuatayo budi yaangaliwe:

- Wanakikundi wanatakiwa kutojiunga kwenye kikundi kabla hawajapata jibu la kwa nini, na kama kweli kikundi kinahitajika.
- Kikundi kiundwe kama kweli kinahitajika
- Suala la msingi ni kuwa kikundi kinatakiwa kuundwa na watu wanaoona umuhimu, na kwa kuzingatia mazingira yaliyopo na kwa nia ya kutatua tatizo kwa njia ya kuwa kwenye kikundi

## 2.2 Mambo ya kuangalia katika uundaji

Kabla ya kuunda kikundi uchambuzi wa maswali yafuatyo yanatakiwa kuangaliwa kwa kina/undani zaidi na yaweze kujibiwa kama ifuatavyo:

- Je wana uzoefu wa kufanya kazi pamoja?
- Je ni sifa na tabia gani ambazo mwanakikundi anapaswa kuwa nazo?
- Je wanaishi karibu au mbalimbali?
- Je, wangependa kufanya kazi pamoja?

- Je, upo utaalamu wa kutosha wa kuziendesha kazi za kikundi kwa mafanikio?
- Je, wanamudu kiasi gani kupata mahitaji ya shughuli wanayotaka kuanzisha?
- Kila mwanachama achangie kiasi gani?
- Kuna haja ya kukopa?

***Angalizo:*** *Maswali k ama h aya yanachangia k ujenga m singi wa kupata aina ya wanakikundi watakaokubalika kuunda na kukiendesha kikundi Katika kuanzisha kikundi, hakuna idadi inayopendekezwa bali hutegemeana na maamuzi ya wananakikundi na pia kutegemeana na shughuli inayofanyika.*

## 2.3 Ukuaji wa kikundi

Kikundi kinapoundwa mara nyingi huwa kuna maswali mengi sana kwa kila aliyeamua kujiunga. Na daima maswali huwa ni namna gani tatizo litashughulikiwa kwa muda mfupi na haraka kwa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, katika kupata msimamo mzuri lazima kikundi kipitie katika hatua tofauti za msingi kama zinavyofafanuliwa:

**Hatua ya 1: Kuunda kikundi**
Taratibu za kikundi huwekwa, maswali mengi hujitokeza kama vile kwa nini kuunda kikundi na ni nani watakuwa wanachama?

**Hatua ya 2: Misuguano**
Kila mwanakikundi anakuwa na mtizamo tofauti/na mwelekeo wake. Kunakuwa na tofauti ya mahitaji hali ambayo hupelekea kutoelewana kati ya wanakikundi na baadhi kutokuendelea na kikundi

**Hatua ya 3: Kujiunda upya kwa kikundi**
Kikundi hujiunda upya kufuatia mawazo yaliyotangulia, na mwelekeo hulenga kurekebisha au koundoa tofauti za mwanzo

zilizokuwepo. Kikundi huchambua watu wa kujiunga pamoja na tabia zao, na pia huangalia watu wenye vipaji na walio tayari kukiendeleza kikundi.

**Hatua ya 4: Kufanya kwa vitendo (kutekeleza)**
Wanakikundi wanapopata ufahamu mzuri juu ya umuhimu na lengo likiwa ni la kuendeleza kikundi au wanakikundi, basi hatua hii huwezesha zaidi wanakikundi kuimarika na kuelewana vizuri.

Katika hatua hii ndipo unaweza kuwapata watu na vipaji vyao katika kikundi kama vile:

- Washauri
- Wawezeshaji
- Watazamaji
- Watunza muda
- Watuliza ghasia
- Viongozi

**Changamoto**
*Baada ya kufundishwa hatua za kuunda vikundi washiriki walitakiwa kuelezea hatua waliyofikia ya uundaji wa vikundi vyao wakioanisha na maelezo yaliyotokana na mpito wa hatua mbalimbali za uundaji na ukuaji wa vikundi.*

*Washiriki walionesha kwamba vikundi vilivyohudhuria warsha karibu vyote viko katika hatua ya kwanza na baadhi ya vikundi vichache viko kipindi cha mpito cha kuelekea hatua ya pili. Kwa ujumla vikundi vilivyoundwa tayari vinatakiwa kufanya marekebisho ili kuweza kufikia hatua ya 4 na kwamba kila kikundi kinapoanzishwa mara nyingi hupitia hatua zote nne.*

*Suala la msingi la kuangalia, ni kwamba kikundi hakiundwi kwa siku moja bali huundwa na kusambaratika na kujiunda upya kama sehemu ya hatua za mpito na maendeleo ya kikundi*

### 2.4 Uundaji wa mtandao

Vikundi vilivyopitia hatua nne zilizotajwa hapo juu ni vikundi vizuri na vyenye msingi mzuri ambavyo hujenga mtandao ulio imara. Vikundi hujiunga pamoja kwa njia ambayo hufanya kuwepo na mahusiano kati yao ambapo wataweza kujifunza kila mmoja kutoka kwa wenzake, kuchukua hatua za pamoja, kutafuta na kutumia rasilimali pamoja kwa ajili ya kuleta maendeleo na mabadiliko katika jamii.

Ili kujenga mtandao imara lazima:

- Vikundi imara ndiyo viunde mtandao
- Kuwepo na michango toka kwa wanakikundi wanaounda mtandao
- Kuwepo kwa wawakilishi katika mtandao
- Kuchagua viongozi wa mtandao

*Ikumbukwe kuwa mabadiliko yataletwa na sisi wenyewe. Ili kuleta mabadiliko haya katika vikundi ni muhimu kuwepo na nguvu za pamoja kwa kutumia vikundi mbalimbali kadiri ya mahitaji na malengo.*

# 3.0 MISINGI YA VIKUNDI BORA

Kikundi kitakuwa bora iwapo utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za kikundi umepangwa vizuri na kila mwanakikundi anatekeleza wajibu wake ipasavyo katika kukiendeleza kikundi.

**Kikundi imara**

Kikundi imara ni kile kilichoanzishwa na wakulima kwa matakwa yao wenyewe bila kupata msukumo wa mtu yeyote kutoka nje. Wanakikundi wenyewe lazima wawe na lengo ambalo ndilo linaweza kuwafanya waungane kwenye vikundi.

Picha zilizopo kwenye Kiambatisho Na 2 zinaonesha jinsi ambavyo watu wanapokutana kwa mara ya kwanza wanakuwa na mawazo/malengo tofauti bila kumshirikisha mwingine.

**Malengo ya kikundi**

Malengo ya kikundi ndiyo matarajio ya wanachama ambayo wanategemea kuyafanya wakiwa pamoja katika kikundi kwa manufaa ya kikundi kizima. Itakuwa vigumu kuwa na kikundi kama wanachama watakuwa na malengo yanayotofautiana.

*Angalizo*:

*Wanakikundi lazima wapendane na kuaminiana. Upendo kati yao utawale ili kupunguza hali ya malumbano kati ya wanakikundi ili kusaidia kutatua matatizo kwa pamoja na shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.*

# 4.0 UONGOZI BORA WA KIKUNDI

Uongozi ni utaratibu unaowekwa ili kusaidia, kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za kikundi. Katika kuweka misingi imara ya maendeleo ya vikundi, mfumo wa uongozi huhitajika ili kikundi kipate ufanisi katika:

- Kupanga na kuainisha malengo
- Kuwaunganisha wanakikundi
- Kuratibu kazi za kikundi
- Kusimamia mali za kikundi

Uongozi unahusisha viongozi wote wa kikundi ambao ni mwenyekiti, katibu, mweka hazina, na kamati ya kikundi. Kwa hiyo uongozi unatakiwa kudumisha upendo, mshikamano, na kusimamia mambo yote yaliyotajwa. Uongozi wa kidemokrasia hutoa haki sawa ya kushiriki katika shughuli za kikundi kwa viongozi na wanakikundi wake.

### 4.1 Mambo ya kuzingatiwa na uongozi wa kikundi

- Kusikiliza maoni ya wanakikundi
- Kujadili kwa pamoja mambo mbalimbali na kufikia maamuzi kwa pamoja kama vile mipango ya kikundi
- Kuaminiana na kuheshimiana

### 4.2 Sifa za kiongozi

Ili tuwe na ufanisi mzuri katika kuendesha vikundi vyetu ni lazima kuchagua viongozi wenye sifa nzuri kama zifuatazo:

- Awe na moyo wa kujituma na kujitolea
- Awe muwazi na mkweli
- Awe na hekima na uvumilivu
- Awe na tabia ya kuwasikiliza na kutekeleza matakwa ya wanakikundi
- Awe na uwezo wa kujenga mahusiano mazuri kati ya wanakikundi

## 5.0 UENDESHAJI WA KIKUNDI

Uendeshaji wa kikundi hutegemea zaidi kuwepo na usimamizi mzuri wa kanuni kuu au katiba ambayo hutumika kuongoza kikundi na mambo yote yanayohusu kikundi. Katiba huhitajika sana katika kikundi ili itumike kama mwongozo. Katiba hutengenezwa kulingana na mazingira na malengo ya kikundi. Katiba inayotumika ipasavyo na wanakikundi inasaidia kikundi kufikia malengo yaliyowekwa na wanakikundi.

### 5.1 Katiba ni nini?

Ni desturi, kawaida, taratibu zilizo za lazima ambazo zinatumika kama mwongozo katika uendeshaji wa shughuli. Katiba husaidia kuratibu:

- Mwenendo wa viongozi na wanakikundi
- Kazi za kikundi
- Mali ya kikundi
- Haki na wajibu
- Sifa za anayeomba uanachama

Wakati wa kutengeneza katiba inabidi kuzingatia mambo yafuatayo:

- Malengo/madhumuni ambayo kikundi kinatarajia kuyafikia
- Sifa zitakazokubalika ili kujiunga na kikundi na masharti ya kujiunga na viingilio
- Aina ya uongozi wa kikundi, sifa, na muda wa uongozi
- Jinsi ya kuendesha kazi za kikundi
- Ugawaji wa mapato ya kikundi
- Mipaka na maadili ya uongozi

## 5.2 Ushirikishwaji wa wanakikundi

Viongozi wanatakiwa kuwashirikisha wanakikundi katika mambo mbalimbali yanayohusu kikundi ili kuongeza kiwango cha uwajibikaji kwa yale waliyoshiriki kutolea maamuzi. Pia ushirikishwaji wa wanakikundi huongeza mshikamano na kutoa nafasi ya kukosoa na kujikosoa kwa kila mmoja.

Utaratibu mzuri wa kazi za kikundi ni muhimu kuandaliwa ili kurahisisha kusimamia utekelezaji wake. Hii hutegemea sana na kikundi kuwa na kalenda ya kazi ambayo imeandaliwa na wanakikundi wote. Kalenda ya kazi hujumuisha orodha ya kazi zote za kikundi na kuonesha ni lini kazi hizo zitakuwa zimefanyika. Ni muhimu sana kwa kila kikundi kujiwekea utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu kama vile mihutasari ya vikao, kuwepo na daftari la fedha, wageni, mikopo, stakabadhi na leja. Hii hurahisisha kazi ya uandaaji wa taarifa kila zinapohitajika.

## 5.3 Umuhimu wa vikao kwa wanachama

Vikao hutumika zaidi katika kupanga kazi za mwaka na kupitisha bajeti. Wanakikundi wana haki ya kujua mambo yote yanayohusu kikundi ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya kikundi. Ikumbukwe kuwa kuwepo kwa uwazi kunaweza kurahisisha mafanikio ya kikundi, na pia kupunguza malalamiko yasiyo ya msingi kutoka kwa wanakikundi. Vikao vya wanachama ni nafasi ya pekee kwa wanachama kupeana habari kuhusu mambo yanayotokea katika kikundi kama vile kuweka malengo, kutathmini utekelezaji wa kazi, kupanga kazi kwa pamoja, na kupata habari za vikundi vingine au za mtandao.

## 5.4 Idadi ya wanachama katika kikundi

Katika kuunda kikundi, hakuna idadi kamili inashauriwa kitaalamu kama ilivyo kwa shughuli nyingine. Hata hivyo ili kikundi kiwe na mawasiliano mazuri na rahisi yenye maelewano, ni vyema kikundi kiwe na watu wachache ambao ni rahisi kwao kuelewana. Ikiwa wanachama watakuwa wengi sana, ni vigumu kuelewana wakati wa mikutano, na pia kunakuwa na ugumu wa kukusanya michango. Aidha kiwango cha kutegeana kwenye kazi kinakuwa cha juu sana. Hivyo idadi ndogo ya wanachama katika kikundi hurahisisha mawasiliano na kupunguza migongano.

## 5.5 Uwezo wa kikundi

Uwezo wa kikundi ujengwe na wanachama wenyewe bila kutegemea misaada kutoka nje. Ni vizuri kikundi kitumie uwezo wa wanachama wenyewe na rasilimali zilizopo kujenga uwezo wake. Kama ni misaada kutoka nje itumike kama nyongeza ya nguvu ya kile kilichopo ndani ya kikundi. Uwezo wa kikundi hutegemea zaidi michango ya wanachama. Hii ni pamoja na kutoa michango ya hali na mali ili kufanya kikundi kiwe na uwezo wa kujiendesha chenyewe. Mfano, pamoja na kazi mbalimbali za

uzalishaji mali, pia ni muhimu wanachama kuchangia kiasi cha fedha kadiri ya makubaliano kikatiba. Pia njia mbalimbali huweza kutumika ili kutunisha mfuko kama vile kutoza faini kwa wachelewaji wa vikao na kuanzisha miradi midogo midogo ya uzalishaji mali.

### 5.6 Mawasiliano kati ya viongozi na wanavikundi

Viongozi wa vikundi wanatakiwa kuwasiliana na wanachama wao kwa karibu ili kuwezesha pande zote kuelewa vizuri jinsi shughuli za kikundi zinavyoendelea. Hali hii huwafanya wanachama kujiona wanamiliki vizuri chama chao na hivyo migogoro hupungua.

Mawasiliano yanaweza kufanyika kwa kutumia mbinu hizi:

- Mikutano
- Barua
- Kutembeleana
- Kufanya kazi kwa pamoja

# 6.0 TABIA NA MIGONGANO KATIKA VIKUNDI

### 6.1 Maana ya Tabia

Washiriki walibainisha kuwa, tabia ni mwenendo au hali fulani ambayo mtu anaifanya kufuatia mazingira yanayomzunguka bila kujitambua au kuelewa kinachofanyika kwa nia ya kuboresha au kuharibu. Tabia hutegemeana sana na malezi, mazingira, kiwango cha elimu, na mila na desturi zilizopo katika jamii.

Tabia za watu zinaweza kuleta mafanikio au kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa iwapo hakuna udhibiti. Watu wanapokuwa pamoja, kila mmoja hutofautiana na wenzake. Tabia nzuri

huchangia kuleta umoja, ushirikiano, usalama, upendo, uaminifu, utulivu, na uangalifu. Ili kuweza kudhibiti tabia mbovu ndani ya kikundi inabidi kuzitambua na kuzichukulia hatua ili kudumisha umoja na mshikamano. Aina za tabia ni kama:

- Tabia ya kitoto
- Tabia ya kujikweza
- Tabia ya ukorofi
- Tabia ya ubinafsi

Tabia hizi zinaweza kurekebishwa kulingana na mazingira yanayowazunguka kama vile maeneo ya kazi, na hata kupitia vikundi mbalimbali vyenye katiba au sheria za udhibiti mzuri zinasaidia kurekebisha baadhi ya tabia za wanachama, watumishi na wanajamii.

**Tunatakiwa kufanya nini juu ya tabia hizi?**

- Kila mwanakikundi anatakiwa kuelewa tabia ya kila mmoja katika kikundi
- Kila mtu katika kikundi lazima aone kuwa tabia yake inakubalika na inatoa mchango mkubwa kuendeleza kikundi na kwa faida ya kikundi
- Viongozi na wanakikundi ni lazima wakubali kukosolewa dhidi ya tabia zinazoweza kuleta mfarakano ndani ya kikundi

## 6.2 Migongano katika vikundi

Migongano katika vikundi husababishwa na ubinafsi, tofauti kielimu, kutoweka wazi taarifa za mapato na matumizi, uchu wa madaraka na itikadi za kidini. Pindi migogoro inapojitokeza kwenye kikundi ni bora kutatua haraka kabla tatizo hilo halijaota mizizi.

Kwa maneno mengine inapotokea kundi moja au sehemu ya watu katika jamii wakanyimwa nafasi katika kushiriki au kusikilizwa katika kuchangia maamuzi yanayoigusa jamii nzima na watu hao wakigundua kuwa wananyimwa haki basi hali kama hiyo husababisha mlipuko wa migogoro katika jamii hiyo. Mara nyingi migogoro tuliyo nayo ni sehemu ya maendeleo katika jamii kwani matokeo ya marekebisho ya migogoro hufuatia hatua za kimaendeleo.

Migogoro inaweza kuibuka iwapo kuna:

- Ukiukwaji wa taratibu, matumizi ya mabavu katika kuendesha/kutoa maamuzi ya shughuli za jamii
- Matabaka ya kikabila
- Tofauti ya kiuwezo katika nyanja za elimu na umiliki wa rasilimali

Hata hivyo ikumbukwe kuwa ipo migogoro pia ambayo si rahisi kutambulika au kujitokeza. Migogoro hiyo ni pamoja na hofu, kutojiamini, tofauti ya uwezo na kutengwa na jamii. Uzoefu unaonesha kwamba, migogoro isiyojitokeza hasa ndiyo iliyopo katika vikundi vingi na imeleta madhara makubwa ndani ya vikundi hivyo.

Kwa hali halisi maeneo yanayoongoza kusababisha migogoro ni pamoja na:

- Uongozi mbovu
- Mgawanyo mbaya wa rasilimali
- Tofauti katika malengo
- Tofauti za mvuto na utashi.

**Mbinu za kumaliza migogoro**

Ili kumaliza migogoro, mikakati ifuatayo inaweza kutumika kwa kuangalia hali halisi ya tatizo lililopo:

- Suluhisho kwa kutumia mbinu shirikishi
- Usuluhishi kwa kutumia katiba

- Maafikiano
- Kutumia sheria.

# 7.0 WAJIBU WA WANAKIKUNDI NA KAMATI YAO

## 7.1 Muundo wa kamati

Ili kikundi kiwe endelevu inabidi kuwa na wanakikundi wanaojitolea kufanya kazi mbalimbali za kikundi bila kutegemea mwingine. Pia kuwe na kamati inayowajibika katika kuendesha shughuli za kikundi. Ukubwa wa kamati unataegemea idadi ya wanakikundi. Hata hivyo kamati ya kikundi inahusisha wajumbe wafuatao:

- Mwenyekiti
- Katibu
- Mtunza hazina
- Wajumbe

## 7.2 Wajibu wa kikundi

- Kupokea mapendekezo, matatizo, kujadili na kutafutia ufumbuzi wake
- Kufuatilia kwa karibu taratibu zote ndani ya katiba na kuzifuata
- Kufuatilia ili kujua maendeleo ya kikundi
- Kukipenda na kukilinda kikundi
- Kujua na kutekeleza malengo, kanuni, sheria na mikakati ya kikundi
- Kuwa waadilifu/nidhamu
- Kujituma katika shughuli za kikundi kufuatia kalenda ya kazi
- Kuwa kiungo cha kuwajumuisha wanakikundi wote
- Kujumuika na wanakikundi kuunda katiba, na kuitumia



SNAL
DATE
SPECIAL COLLECTION

- Kukabili na kusuluhisha migogoro ya kikundi
- Kutoa michango na viingilio ya kikundi
- Kuchagua viongozi wenye sifa nzuri
- Kubuni, kupanga, na kutekeleza miradi ya kikundi
- Kuheshimu uongozi uliopo
- Kuhudhuria vikao vya kikundi

### 7.3. Wajibu wa kamati ya kikundi

- Kusimamia mgawanyo wa kazi na utekelazaji wake
- Kutoa mwongozo wa utekelezaji wa kazi
- Kuandaa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa kazi na mafanikio ya kikundi
- Kuhakikisha mawasiliano ya karibu yanakuwepo kati ya viongazi na wanakikundi
- Kutekeleza mambo yaliyopitishwa na mkutano wa wanakikundi wote
- Kufanya vikao vya kutathmini maendeleo ya kikundi
- Kutunza kumbukumbu za mikutano na fedha ya kikundi

NB. Kamati inayofanya kazi vizuri husaidia sana kufikia malengo ya kikundi

## 8.0 HITIMISHO

### 8.1 Mpango wa kazi

Ni dhahiri kwamba vikundi vinaweza kufanya vizuri iwapo vitakuwa na mpango wa kazi kwa kipindi cha mwaka mzima. Ni mara chache sana kukuta vikundi vikiwa na mpango wa kazi. Hali hii inachangia sana kufanya shughuli za vikundi kutokuwa endelevu. Kwa kawaida, mpango wa kazi huonesha shughuli zitakazofanyika na wakati zitakapofanyika, kitu ambacho hurahisisha usimamizi na utekelezaji wa majukumu mbali mbali katika vikundi.

Kiambatisho Namba 3 kinaonesha mipango ya kazi watakazozifanya washiriki wa warsha kutokana na elimu waliyopata katika warsha.

## 8.2 Mapendekezo ya kuboresha vikundi

Washiriki walitoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha vikundi:

- Wataalamu watembelee vikundi mara kwa mara
- Kushirikisha taaluma mbalimbali katika kuanzisha na kuendeleza vikundi
- Kuwepo na mtandao wa vikundi wa ndani na nje
- Mafunzo yatakayokuwa yanatolewa yalenge mahitaji muhimu ya vikundi
- Kutoa elimu ya uzalishaji, masoko, uendeshaji na uimarishaji wa vikundi
- Kuwezesha vikundi katika usajili na kuwa na akiba benki

Washiriki pia walitoa maombi yao kama ifuatavyo:

- Mafunzo kwa vikundi vingi zaidi, yatolewe walau kwa mwaka mara tatu
- Ziara za mafunzo mbalimballi ili kujifunza zaidi
- Usafiri upatikane kwa ajili ya maafisa ugani ili waweze kuwafikia walengwa kwa wakati mwafaka
- Siku za kufanya warsha hazitoshi na hivyo wanaomba wawezeshaji waongeze muda kwa warsha zijazo

## 8.3 Tathmini ya warsha

Baada ya warsha tathmini ilifanyika na matokeo yake kwa ufupi ni haya yafuatayo:

| Mambo yaliyofurahisha | Upungufu uliojitokeza |
|---|---|
| Ushirikiano mzuri kati ya washiriki wote, watafiti, wagani, na wakulima | Utaratibu wa mapokezi haukuwa mzuri |
| Warsha ilikuwa nzuri sana, na masomo yote yamefundishwa kwa ufanisi mzuri na kumuelewa mwezeshaji/ufundishaji mzuri wa mwezeshaji | Muda mdogo kwa mafunzo/ siku za mafunzo ni chache sana wakati masomo yanatakiwa kufanyiwa kazi |
| Kupata mafunzo na kujua maana ya kikundi | Muda wa kuandaa chakula ulichukua muda mwingi |
| Kukosoana na kuelimishana kuhusu shughuli za vikundi | Kuchelewa kuanza masomo pale ambapo ukumbi ulichelewa kufunguliwa |
| Upendo ulichukua nafasi kubwa wakati wa warsha | |
| Vichekesho/michezo vilifurahisha | |
| Umuhimu wa kutumia katiba na kalenda ya kazi katika kikundi | |

## 8.4 Kufunga warsha

Warsha ilifungwa na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Mheshimiwa Bwana Elias Goroi, ambaye alifurahishwa na uongozi wa mradi hasa kwa jinsi unavyoweza kukutanisha wakulima, watafiti na wagani katika kutatua matatizo ya wakulima wadogowadogo ambayo ni pamoja na uundaji wa vikundi. Alitoa changamoto kwa miradi mingine kuiga utaratibu huu. Shughuli hii iliambatana na kutoa zawadi kwa Wakulima, Wagani na Watafiti mahiri katika utekelezaji wa mradi kutoka Kanda ya Mashariki na SUA.

## 9.0 VIAMBATISHO


### Kiambatisho Namba 1: Orodha ya washiriki wa warsha

| | Jina | Jinsi | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Batuli H. Kiberenge | Ke | Mkulima | Songabatini | Songabatini | SLP 363, Muheza, Tanga |
| 2. | Constantin Mtamba | Me | Mkulima | Langali | Langali | S.L.P. 1880, Morogoro |
| 3. | David Mwambashi | Me | Mkulima | Vuga Bagai | Vuga | SLP 25, Soni, Lushoto |
| 4. | Elizabeth Mchiro | Ke | Mkulima | Langali | Langali | S.L.P. 1880, Morogoro |
| 5. | Ephraim Magali | Me | Mkulima | Tangeni | Mzumbe | S.L.P. 640, Morogoro |
| 6. | Fatuma Ngahemela | Ke | Mkulima | Idete | Idete | SLP 217, Ifakara, Morogoro |
| 7. | Iddi Selemani | Me | Mkulima | Vuga | Vuga | SLP. 2, Soni, Lushoto |
| 8. | Ingekuwa Mohamed | Ke | Mkulima | Visiga | Visiga | SLP. 30173, Kibaha, Pwani |
| 9. | Manate O. Mchumo | Ke | Mkulima | Mkenge | Mkamba | SLP. Mkuranga, Pwani |
| 10. | Margaret Robert | Ke | Mkulima | Bagamoyo | Bombani | S.L.P. Muheza, Tanga |
| 11. | Modestus Kifyoga | Me | Mkulima | Idete | Idete | SLP. 316, Ifakara, Morogoro |
| 12. | Peter J. Chomba | Me | Mkulima | Songabatini | Songabatini | SLP. 363, Muheza, Tanga |
| 13. | Rehema Yusuph | Ke | Mkulima | Tongwe | Bombani | C/o S/ Msingi Tongwe Muheza, Tanga |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Rukia Mkufya | Ke | Mkulima | Semnghano | Kilulu | S.L.P. 20, Muheza, Tanga |
| 15. | Tabu Bagamika | Ke | Mkulima | Masuguru | Masuguru | S.L.P. 20, Muheza, Tanga |
| 16. | Claud Ligugu | Me | Mghani | Idete | Idete | S.L.P. 217, Ifakara, Morogoro |
| 17. | Thecla Makoko | Ke | Mghani | Visiga | Visiga | S.L.P. 30112, Kibaha, Pwani 0744052758 |
| 18. | Zenobia J. Mtenga | Ke | Mghani | Vuga | Vuga | S.L.P. 2, Soni, Lushoto 0748452999 |
| 19. | Reynold Msangi | Me | HUSETA | Dsm | Dsm | S.L.P. 40912, Kinondoni, DSM |
| 20. | Richard Shebughe | Me | SECAP | Lushoto | Lushoto | SLP. 72, Lushoto, Tanga 0748634937, richshebughe @yahoo.com |
| 21. | Riziki Shemdoe | Me | AHI | Lushoto | Lushoto | S.L.P. 22, Lushoto, Tanga 255 27 2640214, rizikishemdoe @yahoo.com |
| 22. | Aida Magelanga | Ke | Mtafiti | ARI-Uyole | Uyole | S.L.P. 400, Mbeya 0744580083, amagelanga@ yahoo.com |
| 23 | Akwilini J. P. Tarimo | Me | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3035 Morogoro |
| 24. | Daniel Chilosa | Me | Mtafiti | ARI-Cholima | Dakawa | S.L.P1892, Dakawa, Morogoro 0744688665 |
| 25. | Eliakunda | Ke | Mtafiti | ARI- | Uyole | S.L.P. 400, |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kimbi | | | Uyole | | Mbeya 0744371470, cekimbi@yahoo.com |
| 26. | Jeremias G. Mowo | Me | Mtafiti | ARI-Mlingano (AHI) | Mlingano (Lushoto) | S.L.P. 20 Muheza, Tanga S.L.P. 22 Lushoto, jgmowo@yahoo.com |
| 27. | Joyce G. Lyimo-Macha | Ke | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3044, Morogoro 0744368877, joyce@suanet.ac.tz |
| 28. | Philemon M Kawamala | Me | Mtafiti | ARI-Mikocheni | DSM | S.L.P. 6226, DSM pmkawamala@yahoo.co.uk |
| 29 | Rogers E. Malimbwi | Me | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3013. Morogoro |
| 30. | Fausta Valery | Ke | Mwezeshaji | Mbeya | Mbeya | S.L.P.2030, Mbeya 0744091416; fausta_1@yahoo.com |

**Kiambatisho Namba 2: Jinsi watu wanavyokutana kwa mara ya kwanza**



## Kiambatisho Namba 3: Mipango ya utekelezaji wa kazi za vikundi

**Kikundi**: Jitume, **Kijiji**: Mkenge. **Wilaya:** Mkuranga
**Mshiriki:** Manate Omari Mchumo

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Wanakikundi kutoshirikishwa kulingana na makubaliano (Kutowajibika bila sababu yoyote) | Kuona kila mwanakikundi anawajibika na kutekeleza mambo yote kadiri ya maazimio ya wanakikundi | • Kuunda kamati ya nidhamu<br>• Kuitisha kikao cha wanakikundi na kutathmini tabia za wanakikundi na kujadili juu ya uwajibikaji wa kila mwanakikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi wote |
| Kutotumia katiba ingawa ipo | Kuona katiba inatumika ipasavyo na wanakikundi wote | • Kuhimiza kila mwanakikundi na viongozi kutumia katiba ipasavyo<br>• Kuunda kamati tendaji ya kikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi wote |
| Kutojua kusoma na kuandika | Kuona wanakikundi wote wanajua kusoma na kuandika | • Kukubaliana na wanakikundi wote kuhusu kuanza kisomo cha watu wazima<br>• Nitamuomba mume wangu awe mwalimu wa kikundi chetu<br>• Kutuma maommbi ya kufundishwa kwa mwalimu mkuu shule ya mkenge | Julai 2004 2004 na kuendela | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi wote<br>• Wataalamu<br>• Mwenyekiti/katibu wa kijiji |
| Kukosa elimu ya kutunza kumbukumbu | Kuona wanakikundi wote wanajua kutunza kumbukumbu | • Kupeleka maombi ofisi ya ushirika ya wilaya ya Mkulanga ili kupata mtaalamu wa kkutoa mafunzo<br>• Kufanya mafunzo ya utunzaji wa aina mbalimbali za kumbukumbu ngazi ya kikundi | August 2004 na kuendelea | • Kamati<br>• Wataalamu |

**Kikundi**: MUWAMU, **Kijiji**: Michungwani. **Wilaya:** Muheza
**Mshiriki:** Rukia Mkufya na Tabu Bagamika.

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kutojua kusoma na kuandika | Nataka kuona wanakikundi wote wanajua kusoma na kuandika | • Kuorodhesha wanakikundi wasiojua kusoma na kuandika<br>• Kutafuta walimu wa kufundisha<br>• Kununua vifaa vya kufundishia kama ubao, chaki, madaftari, kalamu<br>• Kuwafundisha wasiojua kusoma na kuandika | • Julai 2004 2004 na kuendelea<br>• Julai 2004 2004 na kuendelea<br>• Augusti 2004 na kuendelea<br>• Augusti 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Kamati ya kikundi<br>• Kamati ya kikundi<br>• Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu |
| Wanakikundi kutotumia katiba | Kuona katiba inatumika kikamilifu na wanakikundi wote | Kuitisha vikao vya wanakikundi wote ili kuwaelimisha kuhusu matumizi mazuri ya katiba katika kikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | Kamati Wanakikundi |
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona vitabu vya kumbukumbu zote ziwe zinatumika kama daftari la fedha, madeni, mahudhurio, na wageni | • Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu<br>• Kutengeneza vifaa vya kutunzia kumbukumbu | • Julai 2004 na kuendelea<br>• August na kuendelea | • Mtaalamu wa maendeleo ya jamii<br>• Wanakikundi<br>• Kamati ya kikundi |

**Kikundi**: KIWAMIPA, **Wilaya:** Muheza
**Washiriki:** Peter J. Chomba na Batuli H. Kiberenge

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kutokuwa na kalenda ya kazi | Kuona kalenda ya kazi inafuatwa | Kuitisha wanakikundi na kupanga kalenda ya kazi | Julai 2004 – Augusti 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |
| Kutokutumia katiba ya kikundi | Kuona katiba inatumika na wanakikundi wote | Kuitisha mkutano wa kuandaa katiba na kuifuata | Augusti – septemba na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |
| Kukosa ubunifu wa miradi mbalimbali katika kikundi | Kuona miradi mbalimbali inafanywa na wanakikundi | • Kubuni na kuanzisha miraadi ya ufugaji wa kuku, mbuzi, na mingineyo<br>• Kufanya mafunzo ya ubunifu na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi | Septemba – Novemba na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu |
| Kutokuwa na elimu ya kutunza kumbukukmbu | Kuona kikundi kina aina mbalimbali za kumbukumbu kama daftari ya wageni, mahudhurio na mihutasari, na fedha | • Kufanya mafunzo ya kutnza kumbukumbu<br>• Kununua madaftari 3 ya kutunzia kumbukumbu za wageni, mahudhurio na mihutasari ya vikao na daftari la fedha | • Julai 2004 2004 na kuendelea<br>• Julai 2004 – Augusti na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu<br>• Kamati ya kikundi |

**Kikundi: Mkombozi,** Kijiji: **Vuga.** Wilaya: **Lushoto**
**Washiriki**: Wanakikundi

| TATIZO LA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kutokuwa na kamati ya kikundi | Kuona kamti ya kikundi inafanya kazi kufuata katiba ya kikundi | Kufanya kikao cha wanakikundi ili kuchagua wajumbe wa kamati ya kikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | Viongozi wa kikundi Wanakikundi wote |
| Kutokuwa na baadhi ya vitabu vya kutunzia kumbuku mbu | Kuona kuwa vitabu vinapatikana na kutumika kwa ajili ya wageni, mihtasari na mahudhurio, na cha kutunzia fedha | • Kuhamasisha michango ya wanakikundi ili kununua vitabu vya kutunzia kumbukumbu<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu kwa ajili ya wageni, fedha, na mahudhurio na mihutasari | Augusti 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Katibu na mtunza hazina |
| Kukosa ubunifu wa miradi ya kikundi | Kuona kuwa wanakikundi wana miradi ya kiuchumi mbalimbali iliyo endelevu | • Kutuma maombi kwa wataalamu juu ya kupatiwa mafunzo ya ubunifu wa miradi<br>• Kufanya mafunzo ya jinsi ya kubuni na kuendeleza miradi ya kiuchumi | August – septemba 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi/uongozi wa kikundi<br>• Wataalamu wa maendeleo ya jamii/ kilimo/ ushirika<br>• Wanakikundi |

**Kikundi**: TWABAHA, **Kijiji**: Langali. **Wilaya:** Mvomero
**Washiriki:** Elizabeth Mchiro na Costantini Mtammba

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kutokuwa/kukosa kalenda ya kazi | Kuona kuwa kuna mpangilio mzuri wa kazi katika kikundi | • Kununua makaratasi mazito ya kuandalia mpango wa kazi<br>• Kufanya mkutano wa wanakikundi ili kuandaa mpango wa kazi/kalenda ya kazi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |
| Kutokuwa wabunifu wa miradi mingine | Kuona kuwa kuna miradi mingine katika kikundi | • Mafunzo ya ubunifu wa miradi mbalimbali<br>• Kuanzisha biashara ndogondogo<br>• Kutumia wanakikundi wenye vipaji na wabunifu kufundisha wengine kupitia kila kikao | Julai 2004 2004 na kuendelea<br>Septemba na kuendelea<br>Septemba na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Afisa ugani<br>• Wanakikundi |
| Utunzaji wa kikundi usioridhisha | Kuona kuwa kuna vitabu vya aina mbalimbali vya kkutunzia kumbukumbu vinatumika kama daftari la wageni, fedha, uzalishaji, mahudhurio na mihutasari | • Kufanya mafunzo ya kutunza kumbukumbu kwa wanakikundi<br>• Kutengeneza kisanduku cha kutunzia kumbukumbu | Octoba na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu |

**Kata**: Visiga. **Wilaya:** Kibaha
**Mshiriki:** T.F. Makoko – Afisa Ugani

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kikundi kina vitabua vya aina mbalimbali vya kutunzia kumbukumbu kama vile; Daftari la wageni, fedha, uzalishaji, mahudhurio, na mihutasari ya vikao | • Kuhamasisha upatikanaji wa fedha za kununulia vitabu mbalimbali vya kuandikia kumbukumbu kwa kila kikundi<br>• Kufanya mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu<br>• Kununua vitabu mbalimbali na kuvitumia<br>• Kutengeneza kifaa cha kutunzia kumbukumbu | Julai 2004 2004<br><br>Augusti 2004 na kuendelea<br><br>Julai 2004 2004 na kuendelea<br><br>Augusti 2004 – Desemba na kuendelea | |
| Kutojua kusoma na kuandika | Kila mwanakikundi anajua kusoma na kuandika | • Kufanya mkutano wa makubaliano na wanakikundi juu ya kuanzisha darasa la watu wazima ndani ya kikundi<br>• Kufungua darasa la elimu ya watu wazima ndani ya kikundi<br>• Kuandaa ratiba ya kusomana kuandika mara mbili kwa mwezi | Julai 2004 2004 – Desemba na kuendelea | Afisa ugani na elimu |
| Elimu duni ya uendeshaji wa kikundi | Vikundi endelevu na vyenye shudhuli | Mafunzo kwa vikundi juu ya uendeshaji wa vikundi, kubuni | Julai 2004 – Augusti 2004 na kuendelea | • Maafisa ugani toka ushirika,kilimo, mifugo, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | mbalimbali za maendeleo | miradi inayolenga kujitegemea na kikundi kuwa endelevu | | na maendeleo ya jamii |
| Utegemezi uliokithiri | Kuona kila kikundi kimejitegemea na kutumia rasilimali zilizopo katika kujiendeleza | Kufanya mikutano ya uhamasishaaji juu ya umuhimu wa matumizi ya rasilimali zilizopo ili kutunisha mapato ya kikundi kama msingi wa kujitegemea | Julai 2004 – Desemba 2004 na kuendelea | • Maafisa ugani toka ushirika,kilimo, mifugo, na maendeleo ya jamii<br>• Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |

**Kikundi**: Upendo Muungano, **Kijiji**: Bagamoyo Bombani.
**Wilaya:** Muheza
**Washiriki:** Magreth Robert na Rehema Yusufu

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kikundi kina vitabua vya aina mbalimbali vya kutunzia kumbukumbu kama vile; Daftari la wageni, fedha, uzalishaji, mahudhurio, na mihutasari ya vikao | • Kuhamasisha upatikanaji wa fedha za kununulia vitabu mbalimbali vya kuandikia kumbukumbu kwa kila kikundi | Julai 2004 2004 | • Kamati ya kikundi |
| | | • Kufanya mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu | Augusti 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu |
| | | • Kununua vitabu mbalimbali na kuvitumia | Augusti 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi |
| | | • Kutengeneza kabati la kutunzia vitabu vya kumbukumbu | Septemba 2004 – Desemba | • Kamati ya kikundi |
| Kutojua kusoma na kuandika | Kila mwanakikundi anajua kusoma na kuandika | • Kufanya mkutano wa makubaliano na wanakikundi juu ya kuanzisha darasa la watu wazima ndani ya kikundi<br>• Kufungua darasa la elimu ya kujiendeleza ndani ya kikundi na kila mwanakikundi | Augusti 2004 – na kuendelea | • Afisa ugani na elimu<br>• Wanakikundi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | anunue daftari na kalamu<br>• Kuandaa ratiba ya darasa<br>• Kuomba wataalamu wa kufundisha | | |
| Kutokuwa na katiba | Kuona katiba ipo na inatumika | • Uhamasishaji wa wanakikundi juu ya kuwa na katiba ya kikundi<br>• Kikao cha uundaji wa katiba ya kikundi | Julai 2004 2004-07-01<br><br>Julai 2004 2004 | • Afisa ugani na elimu<br>• Wanakikundi |
| Mahudhurio hafifu | Kuona wanakikundi wanahudhuria vikao | • Kuitisha mkutano wa kuandaa ratiba ya vikao | June 2004 na kuendelea | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kikundi |
| Kutojua kusoma na kuandika | Kila mwanakikundi anajua kusoma na kuandika | • Kufanya makubaliano na wanakikundi juu ya kuanzisha darasa la watu wazima ndani ya kikundi<br>• Kufungua darasa la elimu ya kujiendeleza ndani ya kikundi Kuandaa ratiba ya darasa<br>• Kuomba wataalamu wa kufundisha | Julai 2004 2004 – na kuendelea | • Afisa ugani na elimu<br>• Wanakikundi |

**Kata**: Vuga. **Wilaya:** Lushoto
**Mshiriki:** Zenobia J. Mtenga

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kikundi kina vitabua vya aina mbalimbali vya kutunzia kumbukumbu kama vile; Daftari la wageni, fedha, uzalishaji, mahudhurio, na mihutasari ya vikao | • Kuhamasisha upatikanaji wa fedha za kununulia vitabu mbalimbali vya kuandikia kumbukumbu kwa kila kikundi<br>• Kufanya mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu<br>• Kununua vitabu mbalimbali na kuvitumia kama daftari la wageni, fedha, mahudhurio, na mihtasari<br>• Kutengeneza vifaa vya kutunzia vitabu vya kumbukumbu | Julai 2004 2004<br><br>Augusti 2004 na kuendelea<br><br>Julai 2004 2004 na kuendelea<br><br>Augusti 2004 – Desemba | • Kamati ya kikundi<br><br>• Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi<br>• Wataalamu<br><br>• Kamati ya kikundi<br><br>• Kamati ya kikundi |
| Kutokuwa wabunifu wa miradi mingine | Kuona wanakikundi wanaweza kubuni miradi na kuianzisha wenyewe | Mafunzo ya ubunifu wa miradi mbalimbali | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Afisa ugani wa ushirika, na maendeleo ya jamii<br>• Wanakikundi |
| Utegemezi uliokithiri | Kuona kila kikundi kimejitegemea na kujitambua | Kufanya mikutano ya uhamasishaji na kuwaelimisha wanakikundi wajue kuwa kikundi ni chao na wajue malengo ya kikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Maafisa ugani toka ushirika, na maendeleo ya jamii<br>• Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |

**Kikundi**: MWAMKO, **Kijiji**: Visiga. **Wilaya:** Kibaha
**Washiriki:** Wanakikundi

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kutojua kusoma na kuandika | Kila mwanakikundi anajua kusoma na kuandika | • Kuorodhesha wanakikundi wote wasiojua kusoma na kuandika<br>• Kufanya mkutano wa makubaliano na wanakikundi juu ya kuanzisha darasa la watu wazima ndani ya kikundi<br>• Kutafuta waalimu wa kufundisha<br>• Kutafuta vifaa vya kufundishia<br>• Kufungua darasa la elimu ya kujiendeleza ndani ya kikundi Kuandaa ratiba ya darasa | Julai 2004 2004 – na kuendelea | • Afisa ugani na elimu<br>• Wanakikundi |
| Kutotumia katiba | Kuona wanakikundi wanielewa katiba na kuitumia ipasavyo | Kuitisha mkutano wa kkuelezea umuhimu wa katiba | Julai 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |
| Wanakikundi kukosa kalenda ya kazi | Kuona kila mwanakikundi anafanya kazi za kikundi kufuata kalenda ya kazi | Kuitisha mkutano wa wanakikundi ili kuandaa kalenda ya kazi ya kikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamati ya kikundi<br>• Wanakikundi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kikundi kina vitabua vya aina mbalimbali vya kutunzia kumbukumbu kama vile; Daftari la wageni, fedha, mahudhurio, na muhutasari ya vikao | • Kuhamasisha upatikanaji wa fedha za kununulia vitabu mbalimbali vya kuandikia kumbukumbu kwa kila kikundi<br>• Kufanya mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu<br>• Kununua vitabu mbalimbali na kuvitumia kama daftari la wageni, fedha, mahudhurio, na mihtasari<br>• Kutengeneza mahali pa kuhifadhia kumbukumbu | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Kamat ya kikunc<br>• Wanal kundi<br>• Wataa mu |

**Kikundi**: UPENDO, **Kijiji**: Idete. **Wilaya:** Kilombero
**Washiriki:** Wanakikundi

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kikundi kukosa katiba | Kuona katiba ipo na inatumika na wanakikundi wote | Kuitisha kikao cha kuunda katiba | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Viongozi w kikundi<br>• Wanakikun |
| Kutokuwa na uongozi wa kudumu | Kuona kikundi kina viongozi waliochaguliwa wa kudumu | Kuitisha kikao cha kuchagua uongozi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Viongozi w kikundi<br>• Wanakikun<br>• Afisa ugani |
| Mahudhurio hafifu ya wanakikundi | Kuona wanakikundi wanahudhuria vikao na kazi za kikundi | Kuitisha mkutano wa kuandaa kalenda ya kazi na ratiba ya vikao inayoeleweka | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Viongozi w kikundi<br>• Wanakikun<br>• Afisa ugani |
| | | | | |

**Tarafa**: Ifakara. **Wilaya:** Kilombero
**Mshiriki:** Ligulu – Afisa Ugani

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Ushirikishwaji mdogo wa wanavikundi kwenye maamuzi | Wanakikundi wanashirikishwa kwenye maamuzi | Kufanya mikutano ya mara kwa mara ya wanakikundi | Julai 2004 2004 na kuendelea | • Afisa ugani<br>• Wanavikundi wote |
| Mahudhurio hafifu ya wanakikundi | Kuona wanavikundi wote wanahudhuria vikao kama vilivyopamngwa | Kufanya mikutano ya kutengeneza kalenda ya kazi | June 2004 na kuendelea | • Wanavikundi<br>• Afisa ugani |

**Kikundi**: JUHUDI, **Kijiji**: Tangeni. **Wilaya:** Morogoro
**Mshiriki:** Magali

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTAKIWA | KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Kikundi hakina katiba | Kuona katiba ipo na inatumika na wanakikundi wote | Kuitisha kikao cha kuunda katiba ya kikundi | Julai 2004 na kuendelea | • Viongozi wa kikundi<br>• Wanakikundi |
| Kutokuwa na uongozi wa kudumu | Kuona viongozi wa kudumu wamechaguliwa | Kuitisha kikao cha kuchagua viongozi | Julai 2004 2004 | • Wanakikundi |
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kuna vitabu vya kumbukumbu na vinavyotumika | Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu | Augusti na kuendela | • Wanakikundi<br>• Afisa ugani |
| Mahudhurio hafifu ya wanakikundi | Kuona wanakikundi wote wanahudhuria vikao na kazi | Kuitisha mkutano wa kutengeneza kalenda na ratiba ya kazi | Julai 2004 na kuendela | • Wanakikundi<br>• Afisa ugani |

ISBN: 9987-422-06-3